

SOKO LA HISA LA DAR ES SALAAM

TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA TANO WA MWAKA WA WANAHISA

Taarifa inatolewa kwa wanahisa kwamba Mkutano Mkuu wa Tano wa Mwaka wa Wanahisa wa Kampuni ya Soko la Hisa la Dar Es Salaam (Dar Es Salaam Stock Exchange PLC) utakaofanyika katika **Ofisi za DSE, zilizopo Ghorofa ya 3, Jengo la Kambarage, Mtaa wa Ufukoni, Dar Es Salaam** na pia kwa njia ya **Mtandao wa Zoom** (Zoom Teleconferencing), siku ya **Ijumaa tarehe 12 Juni 2020** kuanzia saa tatu na nusu asubuhi (9.30 a.m.) kwa madhumuni yafuatayo:

1. Kupitisha ajenda ya Mkutano;
2. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Nne wa Mwaka;
3. Yatokanayo na Mkutano Mkuu wa Nne wa Mwaka;
4. Kupokea na kupitisha
 - 5.1 Taarifa ya Bodi ya Wakurugenzi ya DSE kwa Mwaka uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2019;
 - 5.2 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya DSE na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2019;
 - 5.3 Taarifa ya Ukaguzi wa Mahesabu ya *Fidelity Fund* na Taarifa ya Mkaguzi wa Nje kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2019;
5. Kupitisha Malipo ya Wakaguzi wa Nje;
6. Uteuzi wa Wakaguzi wa Nje kwa Mwaka wa Fedha 2020;
7. Kuidhinisha Malipo ya Ada ya Wakurugenzi kwa Mwaka wa Fedha 2020;
8. Kuidhinisha Malipo ya Gawio kwa Mwaka Uliyoishia Tarehe 31 Disemba, 2019; na
9. Mengineyo.

Maelezo:

- (i) Kutokana na tishio la janga la ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona (COVID-19), na kufuatana na maelekezo ya wataalamu wa afya yanayotolewa na Serikali kuhusu kuepuka mikusanyiko, wanahisa wanashauriwa kushiriki katika Mkutano kwa njia ya Mtandao wa Zoom, kwa kiunganishi (link) kitakachotolewa kuanzia tarehe 8 Juni 2020.
- (ii) Wanahisa watakaotaka kushiriki katika Mkutano kwa njia ya mtandao, wanatakiwa kutoa taarifa kwa Mwanasheria wa Kampuni kwa njia ya simu na. +255747536696 au kwa barua pepe kupitia info@dse.co.tz or msmniwasa@dse.co.tz kuanzia tarehe 8 Juni 2020 ili kupatiwa kiunganishi cha Mkutano huo:
- (iii) Mwanahisa atakaye hudhuria Mkutano kwenye Ukumbi atatakiwa kufika na nakala ya "*Depository Receipt*" pamoja na kitambulisho chake. Pia atatakiwa kuzingatia maelekezo ya Serikali na Wataalamu wa Afya ya jinsi kujikinga na maambukizi ya ugonjwa unaosababishwa na virusi vya corona. Hii ikiwa ni Pamoja na kuvaa barakoa, kupimwa joto la mwili na kuzingatia umbali wa mtu mmoja hadi mwingine (social distancing).
- (iv) Mwanahisa yeyote anayestahili kuhudhuria na kupiga kura kwenye Mkutano ana haki ya kuchagua mwakilishi au wawakilishi na kupiga kura kwa niaba yake. Endapo mwanahisa ni taasisi/kampuni, mwakilishi anatakiwa kuwa na fomu za uwakilishi ziwe zimegongwa muhuri wa kampuni. Fomu hizo zifikishwe kwa Katibu wa Bodi ya Wakurugenzi katika ofisi za DSE kabla ya saa nane mchana (02:00 p.m.) tarehe 9 Juni 2020.
- (v) Mwanahisa anaweza kumteua Dalali wa Soko, mmoja wa Wakurugenzi wa DSE (Non-Executive Director), au mmoja wa Wasajili wa Hisa (mfano NMB, CRDB, CAD Securities Ltd au CSD & Registry Co. Ltd) kama mwakilishi. Wanahisa wanahamasishwa kutumia wawakilishi na wanashauriwa kuteua wawakilishi kwa kujaza fomu za uwakilishi.
- (vi) Vitabu vyenye taarifa za hesabu kwa mwaka 2019 pamoja na fomu ya mwakilishi vitapatikana katika Ofisi za DSE, Ghorofa ya 3, Jengo la Kambarage, Mtaa wa Ufukoni na kwa Madalali wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam kuanzia tarehe 1 Juni 2020.
- (vii) Orodha (Register) ya Wanahisa watakaostahili kupiga kura itafungwa Jumatano tarehe 9 Juni 2020.

Kwa Agizo la Bodi

Mary Stephen Mniwasa
Katibu wa Bodi
19 Mei 2020